East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 2, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 2, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uainishaji wa Mbinu na Viwango vya Usimulizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka*

*Kimatwek Betty Chepkogei[1*] Nilson Isaac Opande[1] na Ezra Nyakundi Mose[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kisii, S. L. P. 408-40200, Kisii Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mas166020615@kisiiuniversity.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*12 Desemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Usimulizi, Uhalisia, Ulimwengu mpya na Naratolojia.*

**IKISIRI**

Makala haya yanaainisha mbinu na viwango vya usimulizi katika riwaya ya Kiswahili. Uchunguzi huu ulichanganua riwaya mbili za Kiswahili zilizoteuliwa kimaksudi kwa uchunguzi wa matumizi ya mbinu ya usimulizi kama mtindo wa uendelezaji wa hadithi na utunzi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa. Riwaya zilizoteuliwa ni Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka. Uchunguzi uliongozwa na nadharia ya Naratolojia iliyoongoza uchanganuzi wa mbinu na viwango vya usimulizi vinavyochangia katika uendelezaji wa malengo ya matunzi na utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Usimulizi uliowasiliswa kwa vielelezo vya visanduku vya kichina vilivyowakilisha aina mbalimbali za usimulizi ndani ya usimulizi. Data ilikusanywa na kuchanganuliwa kithamano kutokana na riwaya teule kwa kusoma na kudondoa nukuu muhimu za usimulizi wa viwango mbalimbali. Matokeo ya utafiti yaliasilishwa kimaelezo na kwa michoro kuwakilisha viwango mbalimbali vya usimulizi wa hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu. Utafiti ulibaini kuwa usimulizi katika mtindo wa viwango mbalimbali vya kidaraja ulitumika kujenga umbo la kipekee la hadithi. Usimulizi katika viwango au daraja mbalimbali ulihusisha hadithi ndogo za aina ya visasili zilizosimuliwa ndani ya hadithi kuu ambao ni mtindo wa utunzi wa riwaya mpya ya Kiswahili na mtindo huo ulichangia katika kuendeleza, kukuza na kuhifadhi mbinu za kijadi ya Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi ya kisasa.

**APA CITATION**

Chepkogei, K. B., Opande, N. I. & Mose, E. N. (2023). Uainishaji wa Mbinu na Viwango vya Usimulizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(2), 44-54. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620.

**CHICAGO CITATION**

Chepkogei, Kimatwek Betty, Nilson Isaac Opande and Ezra Nyakundi Mose. 2023. "Uainishaji wa Mbinu na Viwango vya Usimulizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 44-54. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620.

**HARVARD CITATION**

Chepkogei, K. B., Opande, N. I. & Mose, E. N. (2023) "Uainishaji wa Mbinu na Viwango vya Usimulizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 44-54. doi: 10.37284/jammk.6.2.1620.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

**IEEE CITATION**

K. B. Chepkogei, N. I. Opande, & E. N. Mose "Uainishaji wa Mbinu na Viwango vya Usimulizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 44-54, Dec. 2023.

**MLA CITATION**

Chepkogei, Kimatwek Betty, Nilson Isaac Opande & Ezra Nyakundi Mose. "Uainishaji wa Mbinu na Viwango vya Usimulizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Dec. 2023, pp. 44-54, doi:10.37284/jammk.6.2.1620.

**UTANGULIZI**

This paper investigates the use of narration and levels of narration in the construction of the Kiswahili novel. The investigation analyzed two Kiswahili Novels sampled purposively for the use of narration as a stylistic device in the narrative structure and construction of the modern Kiswahili novel. The novels were *Bina - Adamu!* and *Babu Alipofufuka.* The analysis was guided by the theory of Narratology. The theory of Narratology was used to examine the narrative structure by investigating the element of the narratives levels as a technique in dissecting the plot of the narrative in in relation to the Chinese boxes model where the story is told in the form of a narrative inside a narrative to determine their functions and relationship to realize a new modern Kiswahili novel. The researcher reviewed literature about levels of narration in selected novels. Data was collected and analyzed and results presented in an informed discourse. The drawings represented embedded narrative within the primary narrative is a style in the new Swahili novel that contributes to developing and preserving the traditional methods of oral literature in modern written literature. The research revealed that the presentation of narrative in the style of hierarchal narrative levels was used to create a unique form of the story.

## UTANGULIZI

Usimulizi ndani ya usimulizi mwingine hujenga vidaraja vya usimulizi. Katika utunzi wa riwaya ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka,* watunzi K.W. Wamitila na Said A Mohammed waliunga matini yenye rotuba na mvuto kwa msomaji na kumfanya apate ari ya kuendelea kusoma hadithi kwa kuingiza wahusika juu ya wahusika wengine wanaosimulia hadithi nyingine kwenye hadithi kuu. Mbinu ya kujumuisha kipera cha Fasihi Simulizi ya Kiafrika katika uandishi wa riwaya uliondoa uzoefu wa kuwepo kwa msimulizi mmoja katika hadithi kuu na kumchosha msomaji bali kuwepo kwa mhusika msimulizi mwengine huleta ari ya kuendelea kusoma. Hivyo, katika hadithi kuu kunaweza kuwa na hadithi nyingine ndogo. Kenan (1983) anaeleza kuwa katika hadithi kunaweza kuwa na usimulizi wa hadithi nyingine. Hivi ni kusema kuwa katika ploti kuu mtunzi anaweza kuingiza usimulizi wa hadithi nyingine fupi zikisimuliwa na wasimulizi wengine. Daraja ya kwanza husimulia hadithi kuu. Usimulizi wa daraja ya pili uhusisha usimulizi wa matukio yote yanayotokea katika hadithi kuu. Matukio huwa mengi katika hadithi kuu. Hadithi ndogo zilizosimuliwa na wahusika waliotajwa katika hadithi kuu ndizo hadithi za daraja ya tatu.

Simulizi ndani ya hadithi kuu ndizo huzua viwango vya usimulizi vilivyochunguzwa na kuwakilishwa katika makala haya. Uchotaji wa mbinu za kiusimulizi ambapo matumizi ya hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu kama mtindo ambayo ilisheheni katika Fasihi Simulizi ya kujadi imetumika katika uandishi wa fasihi andishi ya kisasa ili kutilia nguvu na kuhifadhi utamaduni wa kusimulia hadithi kutoka kizazi kingine na kujenga uhalisia katika aushi ya binadamu katika ulimwengu mpya.

### Usuli wa Suala la Utafiti

Hali kwamba hadhira inaingiliana na fanani moja kwa moja ambaye ni msimulizi mmoja wa hadithi kuu hufanya hadithi kuwa na wepesi wa kueleweka na kuwa na uwezo wa kumuuliza maswali hufanya masimulizi katika fasihi simulizi kuwa mwepesi. Hali hii ni tofauti na ilivyo katika fasihi andishi na haswa katika riwaya ambapo hakuna mwingiliano wa ana kwa ana kati ya mwandishi na msomaji. Ingawa, riwaya ya kisasa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

imejaribu kupenyeza vipengele vya masimulizi katika kusuka vitushi mbalimbali, ukosefu wa kuwepo fanani na hadhira kwa wakati mmoja ulisababisha kuwa vigumu kwa wasomi wa riwaya kuandamana na waandishi wake katika vipindi mbalimbali vya nyakati ambavyo vinasimuliwa katika riwaya ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka*. Usimulizi wa riwaya zilizoteuliwa kwa uchunguzi zimeshirikisha wasimulizi wengine wa hadithi ndogo ndani ya hadithi. Hali hii ilipelekea baadhi ya riwaya hizi kuchukuliwa kuwa changamano zinazokanganya na kutoeleweka kwa wepesi. Usimulizi unaotumika katika riwaya ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka* ulionekana kuwa changamani unaoweza kumpoteza msomi. Utafiti huu ulinuia kuchunguza viwango vya usimulizi katika riwaya hizi kwa lengo la kuweka wazi mbinu za usimulizi zilizotumika na waandishi wake ili kuwawezesha wasomi kuelewa mifululizo ya visa na matukio yake na hivyo kupata ujumbe wa waandishi wake kwa urahisi.

## NADHARIA YA UTAFITI

Uchunguzi ulielekezwa na nadharia ya Naratolojia ambayo iliwekwa msingi na Plato (429-349BC), mwanafalsafa wa Kiyunani. Waasisi wa nadharia ya Naratolojia aliainisha aina tatu za viwango vya usimulizi. Miaka mingi baadaye Mfaransa Tzvetan Torodov (1969) alioanisha nadharia ya Naratolojia na sayansi ya masimulizi ambayo ilichanganua usimulizi. Mhimili wa kiwango cha daraja ya usimulizi ni mchakato uliotumika na watunzi wa riwaya ya karne ya ishirini na moja ili kubadilisha uzoefu wa kuwepo kwa msimulizi mmoja katika hadithi kuu katika matini na kudhihirisha uwezekano wa kuwa na hadithi ndogo. Nadharia ya Naratolojia(1969) iliyoongoza uchunguzi huu, ilisaidia kudhihirisha kuwa usimulizi wa kidaraja ulitumiwa kuunda umbo la hadithi kimtindo katika sanaa ya fasihi ili kuimarisha ujumbe katika riwaya za Kiswahili. Isitoshe, matumizi ya viwango vya usimulizi kama mtindo katika utunzi wa riwaya na vipera vingine vya Fasihi Andishi ni mbinu ya usimulizi katika Fasihi ambapo usimulizi umekuwepo katika jamii mbalimbali za Kiafrika tokea dahari na huchotwa na waandishi katika vipindi tofauti vya uandishi wao (Mose, 2021). Uchotaji wa mbinu za kiusimulizi za kiafrika kama mtindo kutoka Fasihi Simulizi katika utunzi wa riwaya mpya ya karne ya ishirini na moja hutilia nguvu na kuhifadhi utamaduni wa kusimulia hadithi kutoka kizazi hadi kingine na kujenga uhalisia katika aushi ya binadamu katika ulimwengu mpya.

### Uteuzi wa Sampuli na Mbinu za Utafiti

Utafiti huu uliteua kimakusudi riwaya mbili za *Bina-Adamu! Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka* kama sampuli lengwa katika utafiti huu kwa misingi ya uteuzi wa malengo maalumu. Watunzi wa riwaya zilizoteuliwa kwa uchunguzi waliandika riwaya nyingi lakini hizi ndizo zilizosheheni ukwasi wa mtindo wa usimulizi wa hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu ambazo ni visasili za kijadi.Utafiti ulilenga riwaya husika mbili na ambazo zilitegemewa kutoa taarifa na data zilizohitajika kwa sababu ndizo zilizodhihirisha mbinu ya usimulizi kama mtindo unaojenga uhalisia katika ulimwengu mpya baada ya kufanya usomaji wa awali. Kimsingi,matokeo ya utafiti utawasilishwa kimaelezo. Michoro ilitumika kuonyesha viwango vya usimulizi ikiwasilisha hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu. Riwaya ya *Bina-Adamu!* (2002) na *Babu Alipofufuka* (2001) zilielezea utamaduni wa jamii pana ambayo inapitia mabadiliko mengi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Utafiti ulikusanya data za kuaminika kutokana na riwaya teule zilizosomwa kwa makini na kuchanganuliwa kwa mujibu wa madhumuni mahususi ya utafiti huu. Mbali na kudurusu maandishi, makala, machapisho, na miswada mbalimbali mtandaoni, utafiti ulikusanya data za ziada kutoka maktaba mbalimbali za vyuo kwa ajili ya kupata maelezo zaidi kuhusu nadharia iliyoongoza utafiti huu. Data ilichanganuliwa kulingana na lengo mahususi ya kueleza jinsi viwango vya daraja ya usimulizi(kiwango cha daraja ya kwanza,ya pili na ya tatu) vinavyodhihirisha kuwepo kwa msimulizi anayesimulia hadithi kuu na katika usimulizi huo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

kukawa na mhusika mwengine anayesimulia hadithi ndogo.

**UAINISHAJI WA VIWANGO VYA USIMULIZI KATIKA KUJENGA UHALISIA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI**

Watafiti walidondoa hoja muhimu na kunukuu vifungu kuhusiana na mada ya utafiti katika riwaya husika ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka.* Ukusanyaji wa data ulifanywa ili kupata ufahamu zaidi na dira maalumu kuhusu mada na nadharia ya utafiti. Vilevile, utafiti ulikusanya hadithi ndogo zote zilizotambuliwa katika riwaya mbili zilizoteuliwa kwa ajili utafiti na kuziainisha kwa misingi ya nadharia ya Naratolojia na lengo kuu la utafiti huu na matokeo ya utafiti kuwasilishwa ifuatavyo.

**Usimulizi wa Daraja la Kwanza**

Baada ya usomaji wa kina wa riwaya teule, kulidhihirika kwamba watunzi walikuwa wametumia usimuliaji wa daraja la kwanza. Daraja la kwanza husimulia hadithi kuu ambayo Genette (1980) kwa Kiingereza ameiita ex*tradiegetic*. *Extradiegetic* ni dhana inayorejelea hadithi kuu au hadithi ya msingi. Wasimulizi wa riwaya ya *Bina-Adamu! na Babu Alipofufuka* wanasimulia hadithi msingi zilizomo katika riwaya hizo. Hadithi kuu katika riwaya ya *Bina-Adamu!* ni safari ya binadamu ambayo inafanywa na msafiri kwa jina Jagina. Mhusika Jagina ni msafiri anayetembea katika Bara la Ulaya, inayoishi jana, Asia inayoishi kwa matumaini, na Afrika inayoishi juzi na jana. Mtunzi anamtumia mhusika Jagina ambaye anatembelea nchi za Afrika moja baada ya nyingine na kuona jinsi uongozi mbaya, njaa, vita, ufisadi, na mafarakano yalivyowaangamiza Waafrika ili kuonyesha hali halisi katika ulimwengu mpya. Aliposafiri, alikutana na mambo ya kimazingaombwe na ambayo hayana mantiki. Mhusika Jagina anafika Afrika inayoishi pembezoni mwa kijiji cha utandawazi na ambacho kinakosa matumaini kutokana na unyonyaji unaowafaidi mabepari wanaoishi katika Bustani ya Edeni ya pili. Msafiri mhusika Jagina anaelezwa kuwa Afrika inahitaji mkombozi jasiri atakayekomboa Bara la Afrika. Hadithi kuu ndiyo iliyosimuliwa na msimulizi wa daraja la kwanza ambaye alijulikana kama Jagina. Hadithi kuu ilisimuliwa kwa nafsi ya kwanza umoja.

Riwaya ya *Babu Alipofufuka* ilisimulia mhusika ambaye ni K. K ni mhusika Mwafrika ambaye baada ya kupata cheo aliwapuuza na kuwakandamiza Waafrika. Mhusika mkuu K anajitokeza kama mhusika mwenye tamaa na hata anawadharau wale walio wa karibu na yeye. Mhusika K aliingiliana na wakoloni na kupuuza mila na utamaduni wa Kiafrika. Alishirikiana na wakoloni na mwisho kuiga maisha na tamaduni za kigeni. Msimulizi alimtumia mhusika K ili kuonyesha uhusiano wa Mwafrika baada ya mkoloni. Mhusika K ambaye masimulizi yanamzunguka alisawiriwa kama mhusika mhalifu wa kijamii katika ulimwengu. Mhusika mzuka (babu) alipotambua tabia zake alimpitisha katika safari ngumu ya mafunzo. Mhusika K alipokonywa kila kitu alichokuwa nacho yaani mali, ubwana, na kazi. Adhabu kali ilimtia mhusika K kiwewe na akajinyonga. Hadithi hii ya kimsingi ilisimuliwa na msimulizi katika nafsi ya tatu umoja.

Kwa muhtasari, masimulizi katika daraja la kwanza huwa juu ya hadithi kuu na usimulizi wake. Matukio katika hadithi kuu huhusishwa na mhusika mkuu. Pia, msimulizi alitumia wahusika wengine kujenga hadithi kuu. Katika riwaya ya *Bina-Adamu!* hadithi kuu ni kuhusu binadamu na katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* hadithi kuu ni kuhusu babu aliyefufuka

**Usimulizi wa Daraja la Pili**

Kulingana na Genette (1980), usimulizi wa daraja la pili kwa Kiingereza ni *intradigetic*. *Intradiegetic* ni daraja la chini kidogo katika usimulizi wa hadithi baada ya daraja la kwanza. Usimulizi katika kiwango cha daraja la pili ulihusisha matukio yaliyosimuliwa katika daraja la kwanza. Matukio yote yaliyotokea katika riwaya ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipokufa* yamo katika kiwango cha daraja la pili. Matukio ni mengi yaliyopatikana katika riwaya zilizoteuliwa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

kwa utafiti. Baadhi ya matukio yaliyosimuliwa katika riwaya ya *Bina-Adamu!* Ni pamoja na lile lililosimuliwa katika *Bina-Adamu!* (Uk. 14-20) ambapo mhusika msafiri Jagina akiwa pangoni alikutana na jitu ambalo lina miguu mikubwa ajabu. Ni refu kiasi cha kutoonekana mwisho wake, linanuka harufu mbaya kama ya beberu na mgongoni mwake limeandikwa *UMERO JAPA* lililotoweka ghafla. Mhusika Jagina pamoja na mwelekezi wake mhusika Hannah waliendelea na safari yao kisha walitumbukia mtoni na kujikuta nchi ya Zakongwe ambapo walipata watu wengi waliokuwa wamekusanyika kwenye sherehe wakichoma nyama. Watoto walikuwa wamevalia vipande vidogo vya ngozi huku wakiigiza sauti ya ndege. Mhusika Jagina alisemwa kwamba alibadilika kiajabu na kuwa mtoto.

Muhusika alizuru nchi nyingine ambapo alikumbana na maafa yaliyowapata watu wengi ambao walikuwa wamelemaa mikono na miguu. Ulemavu huu ulitokana na bomu lililorushwa na mhusika P.P. Bomu liliwaua watu wengi na wale walionusurika baadaye walipozaa watoto walikuwa na ulemavu (uk. 48) ili kuwasilisha maudhui ya uharibifu wa mazingira na madhara yake kwa binadamu katika ulimwengu mpya. Sehemu nyingine mhusika Jagina aliyoitembelea ilikuwa imejaa miti na akaona vijana waliokuwa wakipanga magogo ya miti. Kando kidogo ya sehemu palipopangwa magogo palikuwa na majengo ambayo hayakukamilika kujengwa. Msimulizi alieleza kuwa wanaume wote wenye nguvu walisombwa na lile jitu ambalo ndilo lililosababisha majengo hayo kutokamilika (uk. 22-34). Haya ni kati ya matukio mengine mengi yaliyosimuliwa.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* kuna tukio ambalo linasimuliwa ambapo mhusika Mzuka ambaye amesawiriwa kama jini anazungumza na kilembwekeza chake ambaye ni mhusika mkuu K. Mhusika K alisimuliwa kuwa alitembelea Neo-Casino na kukutana na marafiki wake Delpiero, Di Livio, Von Heim na Miyawaza kutoka nchi za kigeni na wanapanga mradi wa KFF (uk. 14-16).

Pia, kuna usimulizi wa tukio lingine ambapo mhusika K alimnyang'anya Sururu mke wake Zuhura Mapozi na jinsi mhusika K alivyomkaribisha Zuhura kwa mapokezi ya kifahari (uk. 54-61). Huu ni usimulizi wa matukio machache kati ya mengine katika hadithi msingi. Visa hivi ndivyo vinavyosimuliwa katika usimulizi wa kiwango cha daraja la pili. Hadithi zimesimuliwa ili kutumiwa kujenga wahusika Jagina na K kuhusu masuala ya uhalisia katika ulimwengu mpya ambapo msimulizi amewatumia marafiki wake K kuonyesha jinsi tabia za kigeni na za kupotosha zinavyoingizwa nchini kwa kupitia miradi kama vile KFF ambapo ilisemwa kuwa watu wataingia wakiwa uchi. Tamaa ya hela na mali ni hali halisi katika jamii za ulimwengu mpya ambayo huvunja ndoa na familia kusambaratika.

### Usimulizi wa Daraja la Tatu

Simulizi ndani ya simulizi ya daraja la pili zilisimuliwa na wahusika waliomo katika daraja la tatu. Genette (1980) anaeleza kuwa usimulizi wa kiwango cha daraja la tatu ni *metadiegetic* - ambao ni usimulizi wa hadithi ndani ya hadithi na ambao ni usimulizi ulioegemezwa katika daraja la pili. Maelezo ya dhana ya usimulizi wa kiwango cha daraja la pili yalishadidiwa na Kenan (ksj) ambaye anaeleza kuwa katika hadithi kunaweza pia kuwa na usimulizi wa hadithi ndani ya hadithi. Mhusika aliyesimuliwa katika hadithi kuu anaweza kusimulia katika hadithi nyingine ndogo ndani ya hadithi kuu. Ndani ya hadithi ya kiwango cha daraja la kwanza na la pili kuna hadithi nyingine ndogondogo ambazo ziliegemezwa ndani ya hadithi kuu.

Riwaya ya *Bina-Adamu!* ilwasilisha hadithi ndogo ambapo mhusika mkuu Jagina alikumbuka hadithi aliyosimuliwa na nyanya wakati alipokuwa kwao nyumbani.Hadithi ndogo ya *Ndege na Kinyonga* ilisimuliwa na mhusika Jagina katika hadithi kuu ya kumhusu binadamu (uk. 26). Mhusika Jagina alisimulia kisa cha *Ndege na Kinyonga* kinachohusu ndege na kinyonga jinsi alivyosimuliwa na nyanya. Kinyonga alitumwa na Muumba aende akamwambie binadamu kuwa ataishi milele na milele. Lakini kwa sababu polepole yake ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

mwendo, ilimchukua Kinyonga muda mrefu kurudi. Muumba alighadhibika na kuaamua kumtuma ndege ambaye angeruka kwa wepesi na kutua alikokuwa akiishi binadamu. Ndege akamwarifu binadamu kuwa atakufa na kuangamia. Huo ndio uliokuwa mwanzo wa kifo.Kisasili hiki kina uhusiano na safari ya mhusika Jagina ili kumhimiza afululize kwa haraka kwani kulingana na Hanna mwelekezi wake, safari hiyo haikuwa na kituo.

Msimulizi asiyejulikana alimsimulia mhusika mkuu Jagina kuhusu *Kisa cha Wotan*, katika riwaya ya *Bina-Adamu! Uk. 35.* Kisa hicho ambacho pia ni kisasili cha wajerumani ni cha muungu wenye nguvu za kiungu. Muungu huu ulikuwa na vita na mfalme wa mashujaa. Muungu huo ulijeruhiwa ulipofumwa kwa mkuki ulipokuwa ukining'inia mtini kama tumbiri. Ulipokuwa mtini bila chakula wala maji uliteseka kwa maumivu na ulishukiwa na nyimbo akilini zilizohusiana na siri ya maisha. Msimulizi alisimulia kuwa muungu huu ulibadilika na kupata ujasiri na kujitokeza kama jini na kuaminika kuwasaidia Wajerumani kushinda vita kwa sababu ya uganga wake. Hadithi ndogo ilisimuliwa ili kumweleza mhusika Jagina kuhusu kilichochochea tabia ya P.P. ya kutupa mizinga na kuharibu jengo katika vita vya Fyura.

Kuna usimulizi wa hadithi ndogo nyingine ambayo mhusika Jagina msafiri anaikumbuka. Ni hadithi ndogo inayohusu *kisa cha mwanamke Pandora*, katika riwaya ya *Bina-Adamu!* Uk. 138 na ambayo ilisimuliwa na mhusika Jagina. Epimetheus alimwonya kakake Prometheus asimwoe Pandora. Onyo liliangukia sikio la kufa na Prometheus akamwoa Pandora. Pale kwenye nyumba yao katika chumba kimoja, Prometheus alikuwa na sanduku ambalo lilihifadhi maovu na matumaini ambapo Prometheus alimwonya mkewe asilifungue lakini siku moja mkewe alipatwa na shauku ya kutaka kujua lililomo na kulifungua. Mkewe alipolifungua sanduku, maovu yote yalitoka na kujaa ulimwenguni na kilichosalia ni matumaini. Hadithi ndogo hiyo ilimkumbusha Jagina nchi alizotembelea zilizokuwa zikiishi kwa matumaini.

Usimulizi wa hadithi ya kuzaliwa kwa mhusika Jagina katika riwaya ya *Bina-Adamu! uk 58* ni mfano wa usimulizi wa kiwango cha daraja la tatu. Mhusika Jagina ambaye ni msafiri aliwasimulia wenyeji wa nchi yake ambayo haijatajwa kuhusu jinsi alivyofanana na babu yake aliyepigwa na radi na kuharibu jicho lake la kushoto. Jagina wa kwanza ambaye ni babu yake aliyefariki kitambo, miaka michache baada ya nchi kupata uhuru. Mhusika Jagina wa pili alizaliwa akiwa na jicho la kushoto ambalo lilikuwa limefungika. Nyanya yake mhusika Jagina akampeleka kwa waganga na baada ya kufanya alivyoagizwa jicho lake hajalifunga tena. Jagina ni mhusika katika hadithi kuu ya kiwango cha daraja la kwanza akisimulia hadithi ndogo kuhusu kuzaliwa kwake.

Vilevile, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, usimulizi wa kiwango cha daraja la tatu uliwasilishwa kupitia mhusika Mzuka ambaye ni babu yake mhusika mkuu K. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka uk 70*, Said A. Mohammed alisimulia kuhusu *Vidole vya mikono na kidole cha gumba.* Mhusika Mzuka alimkumbusha mhusika mkuu K hadithi ambapo vidole vya mkono vinachocheana kuwa vingeenda vikaibe mahali lakini vikahofia kuwa vitashikwa, kidole cha gumba kinajitoa kutoka kwa genge hilo. Hadithi ndogo ya *Vidole vya mikono na kidole cha gumba* ilisimuliwa ili kuonyesha jinsi mtunzi alivyomtumia mhusika K kujitoa katika shtaka ambapo yeye na wengine walituhumiwa kuwageuza watu vipanya vya majaribio katika maisha ili kuonyesha jinsi ambavyo Waafrika wanavyotumika katika majaribio mengi ya kisayansi na inapotumbukia nyongo wengi wa waanzilishi wa majaribio hayo hujitoa kwenye lawama.

Isitoshe, kuna usimulizi wa hadithi ndogo nyingine uliosimuliwa na msimulizi wa hadithi kuu akitumia nafsi ya kwanza umoja. Mwandishi anasimulia kisa cha *Ngamia na msafiri jangwani* (uk. 99). Ngamia kule jangwani alimwomba mwenye hema sehemu atie kichwa tu alale lakini ngamia alipokaribishwa alianza kwa kuiingiza shingo kisha kifua, mguu na mkia na alipouingiza mwili wote mwenye hema alijipata nje. Msimulizi


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

alisimulia hadithi ndogo ya *Ngamia na msafiri* kumithilisha jinsi K alivyojiingiza katika ndoa ya Sururu na Zuhura Mapozi na kuivuruga ndoa yao. Mhusika K kulingana na msimulizi alijiingiza polepole hadi akamtorosha Zuhura na kisha kumnunulia nyumba jijini ili awe karibu naye. Simulizi hiyo inaonyesha jinsi jamii zilivyoyovunjika kutokana na 'mipango ya kando', kumaanisha kutoaminiana baina ya wanandoa.

Dhana ya Maboksi ya kichina ilijitokeza katika usimulizi wa kiwango cha daraja la tatu. Maboksi ya kichina ni kiwakilishi cha muundo wa hadithi au uigizaji ambapo kuna hadithi ndani ya hadithi. Hadithi ndogo zimeegemezwa katika hadithi kuu. Filamu moja iliyoitwa kwa Kiingereza *Chinese box* kule Amerika mwaka wa 1997 ilifafanua dhana hii kwa upana. Mchina kwa jina Paul Theroux alitumia Filamu hiyo kutoa taswira kamili ya hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu. Uigizaji wake ulihusisha harakati za Hong Kong kupokeza uongozi kwa Jamhuri ya watu wa China Juni 30, 1997. Katika ploti ya hadithi kuu kuna hadithi ndogo tisa za viwango tofauti. Mchoro unaofuata unaelezea dhana ya maboksi ya kichina;

**Mchoro 1: Visanduku vya Kichina vinavyowakilisha Hadithi Kuu na Hadithi Ndogo.**




**Asili**; Jahn, M. (2005). Narratology: A Guide to the Theory of Narrative.

Katika *Mchoro 1*, hadithi katika riwaya inawakilishwa na visanduku vya kichina ambavyo ni seti ya masanduku yenye ukubwa uliohitimu kila moja likitoshea ndani ya kisanduku kikubwa kinachofuata. Dhana ya visanduku vya kichina hurejelea muundo wa masimulizi ambapo riwaya husimuliwa kwa namna ya masimulizi ndani ya simulizi. Hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu hutoa msisitizo wa ujumbe kwa kutumia mtazamo tofauti ikisimulia msuko na ploti, matukio tofauti na ya hadithi kuu.

Gennette (ksj) anafafanua usimulizi wa hadithi ndani ya hadithi kuu kwa kutumia mchoro wa visanduku vya kichina katika riwaya kama ifuatavyo;

**Mchoro 2: Viwakilishi vya Visanduku vya Hadithi ndani ya Hadithi..**





**Asili**: Jahn, M. (2005):25 Narratology: A Guide to Theory of Narratology.

*Mchoro 2* unaonyesha wasimulizi na masimulizi ambapo Genette (ksj) anafasiri kuwa hadithi A ni hadithi kuu, hadithi B1 na B2 ni hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu ambayo ni A na hadithi C ni

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

hadithi ndogo ambayo ni sehemu ya B2. Mchoro huu unamaanisha kuwa hadithi kuu A ni ya kiwango cha daraja ya kwanza, hadithi B1 na B2 ni hadithi zilizosimuliwa katika kiwango cha daraja ya pili na C ni hadithi cha kiwango cha daraja ya tatu.

**Mchoro 3: Mchoro Wakilishi wa msimulizi wa hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu.**




A- Msimulizi wa hadithi kuu.

B- Hadithi kuu.

C- Hadithi ndogo.

**Chanzo:** Jahn, M (2021;25): A Guide to the Theory of Narrative.

Genette katika mchoro 3 aliendelea kuelezea zaidi juu ya wasimulizi na masimulizi kwa kufafanua kuwa msimulizi mkuu anasimulia hadithi kuu B na ndani ya hadithi kuu kuna msimulizi mdogo anayesimulia hadithi ndogo C. Basi hadithi B ni ya kiwango cha daraja la kwanza na hadithi C ni ya kiwango cha daraja la pili. Waandishi wa riwaya ya *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka* walijumuisha dhana hiyo ya visanduku vya kichina katika uandishi wa riwaya.

Katika riwaya *ya Bina-Adamu!* hadithi kuu ilisimuliwa na msimulizi wa daraja la kwanza ambaye anajulikana kwa jina Jagina ambaye ni binadamu msafiri. Katika hadithi kuu, kuna hadithi ya kiwango cha daraja la pili ambayo ilielezea matukio ya hadithi ya kimsingi. Hadithi ya kimsingi inasimuliwa kwa nafsi ya kwanza umoja. Ndani ya hadithi kuu kuna hadithi ndogo ambayo imeegemezwa ndani ya hadithi kuu. Hadithi hizi ndogo ndizo za kiwango cha daraja la tatu kwani zinasimuliwa na wahusika ambao wanahusishwa na hadithi ya daraja la kwanza.

Hadithi ya daraja la kwanza inasimuliwa na mhusika Jagina. Mhusika Jagina anasimulia safari yake ulimwenguni na azma yake ya kuwatafuta wahusika huntha watatu ambao hawajulikani walikotokomea. Pamoja na hayo, alitaka kumjua mhusika P.P. Katika daraja hilo la kwanza, matukio yote yalihusiana na daraja la pili - matukio yote kuanzia mwanzo wa safari yake kijijini hadi tamati aliporudi. Usimulizi huo umeegemezwa katika hadithi ya kimsingi. Hadithi ndogo nyingine imejitokeza katika riwaya hiyo teule. Katika usimulizi wa hadithi ndogo ya *Kisa cha Mwanamke mtabiri* kinachopatikana katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* uk.18, ilisimuliwa kuwa mwanamke huyo alitabiri kuwa watakuja watu watatu ambao wametia moto mfukoni. Aliongezea kusema kuwa nyoka mrefu atanyiririka kutoka kisiwani hadi ziwa Sango. Kisa hicho ni kisasili ambacho msimulizi alikisimulia ujio wa wakoloni na harakati za ujenzi wa reli kuanzia pwani hadi bara na usafiri wa garimoshi ili kuwapokeza wasomaji ndipo wapate kupitisha hadi kizazi kijacho.

Kuna kisasili kingine kilichosimuliwa na mhusika Hanna katika riwaya ya *Bina-Adamu!* Hanna ni mhusika aliyemwongoza mhusika Jagina katika safari yake. Kisa hiki kinahusishwa na hadithi kuu


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

ambapo kinasimuliwa kwa nafsi ya tatu ambapo kiwakilishi "a" kimetumika. Kisasili hiki kilifafanua chanzo cha kifo.

Usimulizi wa hadithi ndogo nyingine ya kiwango cha daraja la tatu unasimuliwa na jamaa mmoja ambacho kisasili cha muungu wa vita na mfalme wa mashujaa wafu anayeitwa Wotan Msimulizi alisimulia kwa kutumia nafsi ya tatu ambapo kiwakilishi 'a' kimetumika. Visanduku vya kichina vinawakilisha hadithi kuu na hadithi ndogo katika riwaya ya *Bina-Adamu!* ikidhihirisha viwango vya hadithi kama ifuatavyo;

**Mchoro 4: Muhtasari wa Uwakilishi wa Visanduku wa Hadithi ndani ya Hadithi katika Riwaya ya Bina-Adamu!**




**Asili**: Data ya utafiti kutoka riwaya ya Bina-Adamu! - K.W. Wamitila.

***A*** - *Hadithi ya kimsingi.*

***B*** - *Matukio yote katika hadithi kuu.*

***C 1*** - *Kisa cha mwanamke mtabiri (uk 18)*

***C 2*** - *Kisa cha Mfalme (uk 22).*

***C 3*** - *Kisa cha Wotan (uk 35).*

***C 4*** - *Kisa cha ndege na Kinyonga (uk 26).*

***C 5*** - *Kisa cha mwanamke kugeuka chumvi (uk 53).*

***C6*** - *Kisa cha mwanamke pandora na kisanduku (uk 138).*

Katika *Mchoro 4* wa hapa juu kunaonyeshwa kuwa hadithi A ndiyo hadithi ya kimsingi na B ni sehemu ya hadithi A, hadithi ndogo C1, C2, C3, C4, C5 na C6 ziliegemezwa katika hadithi A. Hivyo basi, msimulizi wa hadithi A ni wa kiwango cha daraja la kwanza, B ni wa daraja la pili na wasimulizi wa hadithi C1, C2, C3, C4, C5 na C6 ni wa kiwango cha daraja la tatu. Huu ni muhtasari wa hadithi ndani ya hadithi kuu katika riwaya ya *Bina-Adamu!*

Vilevile, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kuna viwango mbalimbali vya usimulizi wa hadithi. Riwaya ilianza na msimulizi akisimulia hadithi kuu ambayo ni ya usimulizi wa daraja la kwanza ambapo baba yake mhusika K ni jini kwa jina Mzuka. Kisha kuna usimulizi wa hadithi ya daraja


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

la pili ambapo palisimuliwa matukio mengi. Baadhi ya matukio ya usimulizi ni baina ya mhusika Sururu, mkewe mhusika Bi Zuhura Maposi na mhusika K kuhusu kuvunjika kwa ndoa yao. Katika matukio hayo, mhusika K alikumbuka ujana wake na jinsi alivyomnyang'anya mhusika Sururu mkewe. Katika hadithi ndogo ya *Ngamia na msafiri jangwani, uk. 99* usimuliaji ulifanywa na mhusika Mzuka. Hadithi ilihusu Ngamia na Msafiri. Hadithi ilisimulia katika katika daraja la usimulizi la tatu.

Hadithi ndogo inahusiana na hadithi ya daraja la pili ili kusisitiza jinsi mhusika K alivyojiingiza katika ndoa ya mhusika Sururu na mkewe, mwishowe Sururu alijipata nje ya ndoa yake. Msimulizi anasimulia hadithi ya *Ngamia na msafiri jangwani* kwa nafsi ya kwanza. Hadithi ya *vidole vya mkono na kidole cha gumba* iliegemezwa katika hadithi kuu. Msimulizi alisimulia masimulizi hayo ya kiwango cha daraja la pili kwa kutumia nafsi ya kwanza umoja 'mimi'. Katika hadithi hii ndogo egemezi, msimulizi amewasilisha katika hadithi kuu ili kufafanua uhalisia wa jinsi mwekezaji anavyojiondoa katika mradi ambao umeleta maafa katika ulimwengu mpya baada ya kuwageuza watu vipanya vya maabara na kufanya uovu huu unaofanyiwa jamii ujulikane. Hadithi hii egemezi inadhihirisha jinsi waekezaji wanavyoungana kufanya uovu na kisha wengine kutoroka.

**Mchoro 5: Muhtasari wa Uwakilishi wa Visanduku wa Hadithi ndani ya Hadithi katika Riwaya ya Babu Alipofufuka.**




**Asili**: Data ya utafiti kutoka riwaya ya Babu Alipofufuka - Said A. Mohammed.

***A** – Hadithi ya kimsingi.*

***B** – Matukio yote kwenye hadithi kuu*

***C1** – Hadithi ya vidole vya gumba (uk 70).*

***C2** – Kisa cha ngamia na msafiri (uk 99).*

Katika mchoro 4.4, hadithi A ndiyo hadithi ya kimsingi inayosimuliwa na msimulizi wa kiwango cha daraja ya kwanza. Hadithi B ni usimulizi wa kiwango cha daraja ya pili. C1 na C2 ni hadithi ndogo zilizoegemezwa katika hadithi kuu ambazo ni za kiwango cha daraja ya tatu. Maelezo haya ni muhtasari wa hadithi ndogo ndani ya hadithi kuu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka.*

## HITIMISHO

Utafiti umedhihirisha matumizi ya usimulizi wa ya daraja ya kwanza, ya pili na tatu kama mbinu bunifu ya kujenga usimulizi wa riwaya ya *Bina-Adamu* na *Babu Alipofufuka* ili kupitisha ujumbe uliodhamiriwa na watunzi. Riwaya zilizoteuliwa kwa utafiti huu zilisheheni hadithi za viwango vya daraja mbalimbali vyenye visa na matukio ya kiuhalisia mazingaombwe lakini ndani yake yakiwa yanasawiri maisha ya karne ya ishirini na moja na mafundisho huku ujumbe uliokusudiwa na waandishi ukiwasilishwa katika usimulizi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1620

Ilibainika kwamba kuna hadithi zilizoegemezwa kwa hadithi kuu katika masimulizi. Dhana ya visanduku vya kichina ndiyo iliyokuwa kielelezo cha kuchanganua usimulizi wa hadithi kuu katika riwaya za Kiswahili. Hadithi ndogo hasa za aina ya visasili zilitumika kujenga hadithi kuu. Ilidhihirishwa kuwa hadithi ndogo tegemezi zilitumika kuendeleza hadithi kuu na kufafanua matukio yaliyopelekea hali fulani kuwepo katika hadithi kuu ambamo imetegemezwa kwa kutumia usimulizi kujenga uhalisia katika ulimwengu mpya. Ilibainika pia kuwa kwa kupitia viwango vya usimulizi mbalimbali vya hadithi, simulizi huwa na mvuto ambao humwezesha msomaji kusoma matini kwa undani na ujumbe kueleweka. Ilithibitika kuwa mtunzi wa riwaya aliweza kuingiza hadithi fupi ndani ya ploti kuu ambayo ilisimuliwa na wahusika wengine.

**MAREJELEO**


Genette, G. (1980). *Narrative Discourse; An Essay in Method.*Ithaca: Cornell University Press.

Jahn, M. (2005). *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. Cologne: University of Cologne.Retrieved from: www.uni-koeln.de/ame02.pppn.htm.

Kenan, S. (1983). *Narrative Fiction Contemporary Poetics*. London: Rouledge.

Mohammed, S.A. (2001). *Babu Alipofufuka.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mose, E. N. (2021). *Motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi katika tamthilia ya kiswahili: mfano wa mashetani, pungwa, ngoma ya ng'wanamalundi na mashetani wamerudi* (Doctoral dissertation, Moi University).

Torodov, T. (1969). *Structural Analysis of Narrative: The Morton Anthropology of Theory and Critism. (eds).* New York:W.W. Norton and Company.

Wamitila, K.W. (2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers,